

Kulinda Heshima ya Waumini

326. **Amesema al-Imam Muhammad al-Baqir a.s. katika *Bihar al- Anwar* , J. 74, Uk. 301:**

“Ni faradhi kwa kila Mwislamu kusitiri na kuzificha aibu sabini (70) za Mwislamu mwenzake (*ili kulinda heshima yake*).”

(Makosa na kasoro zake zote zishughulikiwe kibinafsi na wala zisienezwe na kutangazwa kwa watu wengine).

327. **Al Imam ‘Ali ibn Abi Talib a.s.Amesema katika *Bihar al- Anwar*, J. 74, Uk. 165:**

“Kubali msamaha akuombao Nduguyo Mwislamu na kama hakufanya hivyo, jaribu kumvumbulia hivyo.”

328. **Al Imam ‘Ali ibn Abi Talib a.s.Amesema katika *Mustadrak Al-Wasa’il al-Shiah’il-ush-Shiah*, J. 12, Uk. 305 na 14155:**

“Hali mbaya kabisa ya uhaini ni kutoboa habari zilizo siri.”

329. **Al Imam ‘Ali ibn Abi Talib a.s.Amesema katika *Ghurar-ul-Hikam*, Uk. 322:**

“Kumuonya kwako aliyetenda makosa miongoni mwao au mbele ya watu ni kumdhaliisha.” (Inakubidi uongee naye katika faragha).”

330. **Amesema Al-Imam Ja’far as-Sadiq a.s.katika *Al-Kafi*, J. 2, Uk. 192:**

“Katika matendo yote ayapendayo Allah swt, ni kule kumletea furaha Mwislamu kwa mfano: kumshibisha, kumwondolea majonzi yake, au kumlipia madeni yake.”